TANGAZO LA SERIKALI NA. 388 la tarehe 17/5/2024

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 191)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 227(1))*

## KANUNI ZA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA ZA MWAKA 2024

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
MADHUMUNI

4. Madhumuni.

SEHEMU YA TATU
UTAWALA NA MUUNDO WA TAASISI

5. Mamlaka ya Waziri.
6. Majukumu ya Mkurugenzi wa Mazingira
7. Majukumu ya Baraza.

SEHEMU YA NNE
TARATIBU ZA KUWEKA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA

8. Kuandaa na kuwasilisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi.
9. Kupitia na kuidhinisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi.
10. Kuwasilisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi ulioidhinishwa.
11. Kuweka dhamana.
12. Uwekaji wa dhamana si kinga.
13. Marudio ya tathmini ya dhamana.
14. Taratibu za ufungaji wa mradi.
15. Masharti ya kurudisha dhamana.
16. Utaifishaji na utekelezaji wa dhamana iliyowekwa.
17. Taarifa ya uongo.

SEHEMU YA TANO
USIMAMIZI WA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA ILIYOTAIFISHWA

18. Usimamizi wa dhamana iliyotaifishwa.

SEHEMU YA SITA
KAMATI YA UFUNGAJI WA MRADI

19. Kamati ya Ufungaji wa Mradi.
20. Majukumu ya Kamati ya Ufungaji wa Mradi.
21. Uendeshaji wa shughuli za Kamati ya Ufungaji wa Mradi.

SEHEMU YA SABA
HAKI NA WAJIBU WA MWEKEZAJI

22. Mpango wa kina wa ufungaji wa mradi.
23. Uwezeshaji wa mapitio.
24. Uhuishaji wa mpango wa kina wa ufungaji wa mradi.
25. Haki ya Kurudishiwa dhamana.
26. Ukaguzi Binafsi.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA JUMLA

27. Ufuatiliaji wa mradi baada ya kufungwa.
28. Uwajibikaji wa mwekezaji.
29. Kipindi cha mpito.
30. Muda wa dhamana.
31. Kutunza kumbukumbu.
32. Msamaha.
33. Makosa na adhabu.
34. Rufaa.
35. Mamlaka ya kutoa amri, miongozo ya kisera au ya jumla.
36. Dhamana inayosimamiwa na sheria za kisekta.

---

MAJEDWALI

---

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 191)

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 227 (1))*

# KANUNI ZA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Dhamana ya Kuzingatia Masharti ya Mazingira za Mwaka 2024.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Baraza" maana yake ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lililoanzishwa chini ya kifungu cha 16 cha Sheria;

"dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira" au "dhamana" maana yake ni fedha taslimu, amana ya benki au bima inayowekwa na mwekezaji kwa madhumuni ya kuhakikisha ufungaji salama wa mradi, uboreshaji wa eneo la mradi na urejeshaji wa mifumo ikolojia;

"eneo la mradi lililotelekezwa" maana yake ni eneo ambalo limeachwa na mwekezaji mradi baada ya kulitumia kutekeleza mradi wake bila kulirudisha katika hali inayokaribiana na hali yake ya awali au kulibadilisha katika matumizi rafiki kwa mazingira;

"Kamati ya Ufungaji wa Mradi" maana yake ni Kamati

iliyoundwa chini ya kanuni ya 19;

"mifumo ya usimamizi wa mazingira" maana yake ni michakato na taratibu zinazomwezesha mwekezaji kulinda, kuhifadhi na kutumia kwa njia endelevu sehemu ya mazingira ili kutekeleza mradi kwa ufanisi na kupunguza athari za mazingira;

"Mkurugenzi wa Mazingira" maana yake ni kama iliyoainishwa chini ya Sheria;

"Mpango wa kina wa ufungaji wa mradi" maana yake ni Mpango wa awali wa ufungaji wa mradi uliohuishwa au kuandaliwa wakati wa awamu za ujenzi au uendeshaji na baada ya uendeshaji wa mradi;

"mradi" maana yake ni shughuli au mchakato ambao unahitaji kuwekewa dhamana;

TS. Na. 267 la 2021

"mtaalamu wa mazingira aliyesajiliwa" maana yake ni mshauri elekezi aliyethibitishwa na kusajiliwa chini ya Kanuni za Usajili wa Wataalamu wa Mazingira kwa madhumuni ya kufanya tathmini ya athari kwa mazingira au ukaguzi wa mazingira;

"mwekezaji" maana yake ni mtu ambaye anatekeleza mradi ambao dhamana inaweza kuhitajika;

"Rejista" maana yake ni mfumo wa kumbukumbu za taarifa za wataalamu wa mazingira waliosajiliwa, miradi na dhamana za kuzingatia masharti ya mazingira zilizowekwa na kutunzwa na Baraza;

Sura ya 191

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taratibu bora za kulinda na kuhifadhi mazingira" maana yake ni taratibu ambazo zipo kwa mujibu wa masharti ya Sheria au sheria nyingine yoyote;

"tathmini ya athari kwa mazingira" maana yake ni kama ilivyoainishwa chini ya Sheria;

"tathmini ya dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira" au "tathmini ya dhamana" maana yake ni tathmini ya gharama za ufungaji wa mradi, uboreshaji wa eneo la mradi, urejeshaji wa mfumo ikolojia na usimamizi na ufuatiliaji baada ya kufunga mradi;

"urejereshaji" maana yake ni kurejesha katika hali ya awali, kusafisha na kuendelea kutunza mazingira katika eneo la mradi;

"ufuatiliaji baada ya kufunga mradi" maana yake ni ufuatiliaji endelevu au wa mara kwa mara wa athari halisi au zitakazojitokeza kwa muda mfupi au mrefu katika eneo la mradi au eneo lolote la mazingira lililoathiriwa baada ya kufungwa kwa mradi;

"ufungaji salama wa mradi" maana yake ni ufungaji wa mradi unaolinda na kuzingatia masharti na viwango vya ubora wa mazingira;

"ukaguzi wa mazingira" maana yake ni tathmini ya mazingira inayofanyika hatua kwa hatua katika vipindi maalumu kwa madhumuni ya kuangalia na kufuatilia uzingatiaji wa taratibu bora za kulinda na kuhifadhi mazingira katika eneo la mradi;

"ukaguzi binafsi" maana yake ni kama ilivyoainishwa chini ya Sheria;

"viwango" maana yake ni kama ilivyoainishwa chini ya Sheria; na

"Waziri" maana yake ni kama ilivyoainishwa chini ya Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## MADHUMUNI YA KANUNI

Madhumuni ya Kanuni hizi

4. Madhumuni ya Kanuni hizi ni kutoa na kukuza mazingira endelevu kwa kuhakikisha-

(a) dhamana ya usalama na ubora wa mazingira; na

(b) uzingatiaji wa ufungaji salama wa mradi, uboreshaji wa eneo la mradi na urejeshaji wa mifumo ikolojia wakati na baada ya kufungwa kwa mradi.

## SEHEMU YA TATU
## MUUNDO WA KIUTAWALA NA KITAASISI

Mamlaka ya Waziri

5. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, Waziri atakuwa na mamlaka ya-

(a) kuamua aina ya dhamana ya kuzingatia masharti

ya mazingira itakayowekwa, ambayo inaweza kuwa-
(i) akaunti ya usimamizi;
(ii) amana ya benki;
(iii) dhamana ya mtaji; au
(iv) amana au dhamana yoyote inayokubalika; and

(b) kutoa cheti cha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira.

Majukumu ya Mkurugenzi wa Mazingira

6. Mkurugenzi wa Mazingira atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuratibu na kuhamasisha masuala yote yanayohusudhamana;
(b) kupendekeza motisha za kifedha zinazofaa ambazo zinaweza kuhamasisha jumuiya ya wafanyabiashara kuanzisha bima na bidhaa za kibenki zinazoweza kusaidia wawekezaji kudhibiti vihatarishi vya mazingira vinavyoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi;
(c) kupokea mpango wa kina wa ufungaji wa mradi ulioidhinishwa na Baraza ambao utajumuisha dhamana itakayowekwa;
(d) kumshauri Waziri kuamua aina ya dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira itakayowekwa;
(e) baada ya kupokea uthibitisho wa dhamana iliyokusudiwa kuwekwa, kumshauri Waziri kutoa cheti cha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira;
(f) kulitaarifu Baraza kuhusu kupokea au kutokupokea dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira;
(g) kutunza uthibitisho wa uwekaji wa dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira;
(h) kupokea mapendekezo ya Baraza kuhusu kurudisha au kutaifisha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira; na
(i) kumshauri Waziri kurudisha au kutaifisha

dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira.

Majukumu ya Baraza

7. Baraza litawajibika kusimamia dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira kwa kutekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kutunza rejista ya miradi ambayo imewekewa dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira;

(b) kupitia na kuidhinisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi ili kubaini utoshelevu na usahihi wa maudhui yaliyomo ikiwemo makadirio ya gharama za dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira itakayowekwa;

(c) kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Mazingira mpango wa kina wa ufungaji wa mradi ulioidhinishwa;

(d) kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mwekezaji ambaye hajawasilisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi;

(e) kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Mazingira mapendekezo kuhusu urudishaji au utaifishaji wa dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira;

(f) kupokea taarifa kutoka kwa Mkurugenzi wa Mazingira kuhusu kuzingatiwa kwa uwekaji au kutokuzingatiwa kwa uwekaji wa dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyoamuliwa;

(g) kuchukua hatua stahiki za uzingatiaji na utekelezaji wa kutokuwekwa kwa dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyoamuliwa;

(h) kukagua, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa taratibu za mazingira ili kudhibiti uharibifu wa mazingira kulingana na masharti yaliyoidhinishwa;

(i) kupendekeza kwa Mkurugenzi wa Mazingira kuhusu kurudisha au kutaifisha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyowekwa;

(j) kupitia mpango ya ufungaji wa mradi uliohuishwa na kuwasilishwa na mwekezaji;

(k) kutoa hadidu za rejea kwa Kamati ya Ufungaji

wa Mradi kwa mujibu wa kanuni ya 21;
(l) kuidhinisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi;
(m) kuwasilisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi ulioidhinishwa, kwa Mkurugenzi wa Mazingira kwa ajili ya kuamua na kuidhinisha aina ya dhamana itakayowekwa; na
(n) kutekeleza jukumu lingine lolote lililotolewa chini ya Sheria au sheria nyingine yoyote.

## SEHEMU YA NNE
## TARATIBU ZA UAMUZI NA UWEKAJI WA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA

Kuandaa na kuwasilisha mpango wa kina wa ufungaji wa ramdi

8.-(1) Mwekezaji anayetekeleza shughuli au mchakato wa miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza atatakiwa ndani ya muda ulioainishwa kuandaa mpango wa kina wa ufungaji wa mradi ambao utajumuisha hesabu za makadirio ya dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira itakayowekwa.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mpango wa kina wa ufungaji wa mradi utajumuisha maudhui ya tathmini ya msingi nataarifa za eneo la mradi, uchambuzi wa athari zinazoweza kutokea, vigezo vinavyotumika kutathmini uwezekano wa athari za mazingira katika uso au chini ya ardhi na utakuwa katika namna iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(3) Mpango wa kina wa ufungaji wa mradi utaandaliwa na mtaalamu wa mazingira aliyesajiliwa.

(4) Mwekezaji atatakiwa kusaini tamko lililopo katika mpango wa kina wa kufunga mradi kuthibitisha usahihi wa taarifa zilizotolewa.

Kupitia na kuidhinisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi

9.-(1) Ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kupokea mpango wa kina wa ufungaji wa mradi, Baraza, kupitia kwa Kamati ya Ufungaji wa Mradi, litapitia mpango na baada ya kuridhika na maudhui yake, litaidhinisha au litakataa kuidhinisha mpango huo.

(2) Endapo Baraza halijaidhinisha mpango wa kina

wa ufungaji wa mradi, sababu za kutoidhinisha zitawasilishwa kwa maandishi kwa mwekezaji.

(3) Mwekezaji atatakiwa kuwasilisha tena mpango wa kina wa ufungaji wa mradi ulioboreshwa ndani muda ulioainishwa katika uamuzi wa kutoidhinisha.

Kuwasilisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi ulioidhinishwa

10.-(1) Endapo Baraza limeidhinisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi, litauwasilisha kwa Mkurugenzi wa Mazingira kwa mchakato wa kuamua aina ya dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira itakayowekwa.

(2) Baada ya kuamua aina ya dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira itakayowekwa, Mkurugenzi wa Mazingira atalijulisha Baraza ili, kupitia notisi, limtaarifu mwekezaji kuweka dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira katika namna iliyoamuliwa.

Uwekaji wa dhamana

11.-(1) Mwekezaji atawajibika kuweka dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira kwa Mkurugenzi wa Mazingira kwa mujibu wa notisi iliyotolewa chini ya kanuni ya 10(2) ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kupokea notisi hiyo.

(2) Baada ya dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira kuwekwa, Waziri atatoa kwa mwekezaji cheti cha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira kilichoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(3) Endapo mwekezaji atashindwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1) ndani ya siku thelathini baada ya kuisha kwa muda ulioainishwa, mwekezaji atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni tano na kisichozidi shilingi bilioni kumi.

Uwekaji wa dhamana si kinga

12. Dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyowekwa na mwekezaji kwa Mkurugenzi wa Mazingira haitatumika kama-

(a) msamaha wa kutozingatia masharti ya Sheria, Kanuni hizi, kanuni zozote zilizotengenezwa chini ya Sheria, sheria nyingine yoyote au

viwango vya ubora wa mazingira; na

(b) utetezi katika shauri la madai au mashtaka ambayo yanaweza kuwasilishwa dhidi ya mwekezaji kuhusu namna mradi unavyotekelezwa, kusimamiwa au kuendeshwa.

Marudio ya tathmini ya dhamana

13. Baraza, kupitia Kamati ya Ufungaji wa Mradi, linaweza wakati wowote kurudia tathmini ya kiwango cha dhamana pale ambapo-

(a) kulikuwa na makosa katika tathmini ya dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyofanyika awali;

(b) kuna mabadiliko au marekebisho makubwa katika mradi au namna mradi unavyoendeshwa;

(c) mradi una viashiria vya uharibifu wa mazingira ambavyo havikubainishwa katika tathmini ya mwanzo na vinaweza kuathiri mifumo ikolojia; na

(d) imethibitika kuwa taarifa zilizotolewa na mwekezaji zilikuwa za uongo, si sahihi au zilikusudia kupotosha.

Taratibu za ufungaji wa mradi

14.-(1) Mwekezaji atalitaarifu Baraza kuhusu kusudio la kusitisha uendeshaji wa mradi kwa kuwasilisha taarifa ya uzingatiaji wa mpango wa kina wa ufungaji wa mradi.

TS. Na. 267 la 2021

(2) Mwekezaji atamtaarifu Waziri kupitia Baraza nia ya kurudisha cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira kilichotolewa chini ya Kanuni za Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

(3) Baraza kupitia Kamati ya Ufungaji wa Mradi, ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kupokea taarifa ya uzingatiaji wa mpango wa kina wa ufungaji wa mradi, litakagua mradi ili kuthibitisha uzingatiaji wa masharti, vigezo na viwango vilivyowekwa katika mpango huo.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3), wakati wa ukaguzi katika eneo la mradi, Kamati ya Ufungaji wa Mradi itazingatia yafuatayo:

(a) usalama wa jamii;

(b) ustahimilivu wa eneo la mradi katika hali ya msimu wakilishi wa hali ya hewa ya eneo husika;
(c) urejeshaji wa mifumo ikolojia;
(d) uchambuzi na uchanganuzi wa vigezo vya mazingira vinavyotumika;
(e) kiasi cha muda utakaohitajika kukamilisha ufungaji wa mradi, uboreshaji na urejeshaji wa mifumo ikolojia;
(f) historia ya uzingatiaji ya mwekezaji;
(g) ushirikishwaji wa wadau, jamii inayozunguka na inayoathirika;
(h) masharti, vigezo na viwango vilivyoainishwa katika cheti cha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira; na
(i) kigezo kingine chochote kitakachoamriwa na Baraza.

(5) Baraza, baada ya kujiridhisha kuwa mwekezaji amezingatia viwango vya ubora wa mazingira wakati wa ufungaji wa mradi, litamshauri Mkurugenzi wa Mazingira kurejesha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira.

(6) Dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyowekwa itarudishwa ndani ya kipindi cha muda wa ufuatiliaji baada ya muda wa kufunga mradi ulioainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(7) Mkurugenzi wa Mazingira, baada ya kuridhika na mapendekezo chini ya kanuni ndogo ya (5), atarejesha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira.

Masharti ya kurudisha dhamana
TS. Na. 349 la 2005

15. Mkurugenzi wa Mazingira hatarejesha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira au riba iliyolimbikizwa, kama ipo, isipokuwa pale ambapo cheti cha tathmini ya athari za mazingira kitakapokuwa kimerejeshwa na cheti cha urejeshaji kimetolewa kwa mwekezaji kwa mujibu wa Kanuni za Tathmini ya Athari za Mazingira.

Utaifishaji na utekelezaji wa dhamana

16.-(1) Baraza linaweza, baada ya kumpa mwekezaji fursa ya kusikilizwa kuhusiana na kutotekeleza

iliyowekwa masharti ya Kanuni hizi, kumshauri Mkurugenzi wa Mazingira kutaifisha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyowekwa na mwekezaji.

(2) Baraza litatoa notisi ya maandishi kwa mwekezaji ya kusudio la kutaifisha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira.

(3) Mwekezaji atapaswa kujibu notisi iliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (2) ndani ya siku ishirini na moja kuanzia tarehe ya kupokea notisi hiyo.

(4) Baada ya kupokea majibu ya notisi Baraza litampa mwekezaji fursa ya kusikilizwa.

(5) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (4), Baraza litawasilisha uamuzi wake kwa mwekezaji ndani ya siku kumi na nne.

(6) Endapo uamuzi wa Baraza chini ya kanuni ndogo (5) unahusu notisi ya maboresho kwa mwekezaji ili kurejesha mazingira yaliyoathiriwa, notisi hiyo itabainisha muda wa maboresho.

(7) Endapo mwekezaji atashindwa kutekeleza uamuzi uliotajwa chini ya kanuni ndogo ya (6), Baraza litamshauri Mkurugenzi wa Mazingira kutaifisha dhamana iliyowekwa na itatumika kurejesha mazingira yalioathirika.

(8) Endapo mwekezaji atashindwa kutekeleza matakwa ya sharti la kanuni ndogo ya (3), Baraza litamshauri Mkurugenzi wa Mazingira kutaifisha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyowekwa bila kutoa notisi nyingine.

(9) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (7) na (8), Baraza kupitia Mkurugenzi wa Mazingira, linaweza kumshauri Waziri kufuta leseni, kibali au cheti kilichotolewa kwa mwekezaji chini ya Sheria kwa mradi husika pale ambapo mwekezaji ni mkosaji wa mara kwa mara.

(10) Endapo mwekezaji hajaridhika na uamuzi uliotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (9), anaweza akakata rufaa katika Baraza Rufaa la Mazingira lililoanzisha chini ya Sheria.

Taarifa ya uongo.

17. Mwekezaji anayetoa taarifa za uongo kwa lengo la kupotosha anatenda kos ana akitiwa hatiani atawajibika kwa adhabu ya jumla iliyoainishwa katika Sheria.

SEHEMU YA TANO
USIMAMIZI WA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA ILIYOTAIFISHWA

Usimamizi wa dhamana iliyotaifishwa.

18.-(1) Endapo mwekezaji atashindwa kutimiza masharti ya matakwa yaliyowekwa ya ufungaji salama na uboreshaji wa eneo la mradi, dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyotaifishwa itapaswa kutumika kuboresha mazingira yaliyoathirika.

(2) Baraza litamtaarifu Mkurugenzi wa Mazingira kuhusu ni ya kutumia dhamana iliyotaifishwa kuboresha mazingira yaliyoathiriwa katika eneo la mradi uliositishwa au kutelekezwa.

(3) Baada ya kukamilisha uboreshaji wa eneo la mradi uliositishwa au kutelekezwa, Baraza kupitia Mkurugenzi wa Mazingira, litawasilisha kwa Waziri taarifa inayoonesha hali ya uboreshaji ikiwemo kiwango cha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyotumika katika shughuli za uboreshaji.

SEHEMU YA SITA
KAMATI YA UFUNGAJI WA MRADI

Kamati ya Ufungaji wa Mradi

19.-(1) Baraza litaunda Kamati ya Ufungaji wa Mradi yenye wataalamu wenye taaluma mtambuka ili kupitia na kuchambua mpango wa kina wa ufungaji mradi.

(2) Kamati ya Ufungaji wa Mradi itaundwa na wajumbe kutoka wizara, taasisi za Serikali na taasisi za utafiti na elimu ya juu wenye uzoefu na utaalamu katika mradi unaokusudiwa kufungwa.

Majukumu ya Kamati ya Ufungaji wa Mradi

20. Majukumu ya Kamati ya Ufungaji wa Mradi yatajumuisha:

(a) ukaguzi, ufuatiliaji na tathmini ya uzingatiaji wa viwango vya utunzaji wa mazingira katika eneo

la mradi;

(b) kupitia mpango wa kina wa ufungaji wa mradi;

(c) kurudia tathmini ya dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyowekwa;

(d) kulishauri Baraza kuhusu masuala yanayohusiana na ufungaji wa mradi;

(e) kulishauri Baraza kuhusu usimamizi wa dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira; na

(f) kutekeleza kazi nyingine inayohusu ufungaji wa mradi kama inavyoweza kuelekezwa na Baraza.

Uendeshaji wa shughuli za Kamati ya Ufungaji wa Mradi

21. Katika kutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi, Kamati ya Ufungaji wa Mradi itazingatia hadidu za rejea kama zitakavyotolewa na Baraza.

## SEHEMU YA SABA
## HAKI NA WAJIBU WA MWEKEZAJI

mpango wa kina wa ufungaji wa mradi.

22.-(1) Mwekezaji ataandaa mpango wa kina wa ufungaji wa mradi ambao utajumuisha-

(a) jina na eneo mradi ulipo;

(b) maelezo ya mradi;

(c) cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira au ukaguzi wa mazingira pale inapohitajika;

(d) mifumo ya usimamizi wa mazingira iliyopo;

(e) uboreshaji, urejeshaji wa mifumo-ikolojia na na mpango wa usimamizi wa eneo la mradi utakavyojumuisha viwango vinavyotakiwa vya shughuli za uboreshaji na muda;

(f) taratibu za ufuatiliaji baada ya kufunga;

(g) ufungaji salama endapo kuna dharura pale ambapo itahitajika;

(h) mchanganuo wa mbinu na taratibu mbalimbali za ufungaji salama;

(i) tafiti husika za kisayansi zinazoweza kujumuishwa katika mpango wa kina wa kufunga mradi pale ambapo inalazimu;

(j) ushirikishwaji wa jamii;
(k) mpango wa ufuatiliaji endelevu wakati na baada ya kufungwa mradi;
(l) mchanganuo wa gharama za kiasi cha dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira kitakachowekwa; na
(m) taarifa nyingine inayoweza kuhitajika.

(2) Mwekezaji, ndani ya muda ulioainishwa katika Jedwali la Kwanza, atawasilisha katika Baraza mpango wa kina wa ufungaji wa mradi unaorejewa katika kanuni ndogo (1).

(3) Endapo mwekezaji atashindwa kuzingatia sharti la kanuni ndogo (3), ndani ya siku sitini baada ya kuisha kwa muda ulioainishwa, atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni tano na kisichozidi shilingi bilioni moja.

Uwezeshaji wa mapitio

23. Mwekezaji atatakiwa kutoa uwezeshaji wa kifedha katika mchakato wa kupitia na kuidhinisha mpango wa kina wa ufungaji wa mradi.

Uhuishaji wa mpango wa kina wa ufungaji wa mradi

24. Mwekezaji, ndani ya muda ulioainishwa katika Jedwali la Kwanza, atapitia, atahuisha na atawasilisha mpango wa ufungaji wa mradi uliohuishwa kwa Baraza.

Haki ya kurudishiwa dhamana

25. Mwekezaji atakuwa na haki ya kurudishiwa dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira yote iliyowekwa au sehemu yake, baada ya Baraza kujiridhisha na uzingatiaji wa Kanuni hizi.

Ukaguzi binafsi

26. Mwekezaji atachukua hatua zote zinazowezekana kuhakikisha utekelezaji wa mpango wa kina wa ufungaji wa mradi kwa-
(a) kufanya ukaguzi binafsi kila mwaka;
(b) kuandaa taarifa ya ukaguzi wa mazingira baada ya kila ukaguzi na kuiwasilisha katika Baraza kila mwaka au kama itakavyoelekezwa na Baraza;

(c) kuhakikisha kuwa ukaguzi unazingatia vigezo na masharti yaliyotolewa katika mpango wa kina wa ufungaji wa mradi uliyoidhinishwa na unalenga kuchangia katika ufungaji salama wa mradi.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI YA JUMLA

Ufuatiliaji wa mradi baada ya kufungwa

27. Mwekezaji, ndani ya muda uliotolewa katika Jedwali la Kwanza, atafanya ufuatiliaji na usimamizi wa mwenendo wa athari za mazingira yanayotokana na mradi uliofungwa ili kutathmini uzingatiaji wa masharti ya Kanuni hizi.

Uwajibikaji wa mwekezaji

28. Mwekezaji, isipokuwa kama mradi husika umefungwa kwa usalama, atawajibika kwa viatarishi vyovyote vya mazingira au mabadiliko ya eneo la mradi wakati wa utekelezaji na baada ya kufungwa kwa mradi.

Kipindi cha mpito

29.-(1) Mwekezaji ambaye, kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, anatekeleza mradi ulioainishwa katika Jedwali la Kwanza atatakiwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi ndani ya miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo (1), uzingatiaji wa Kanuni hizi hautaathiri uzingatiaji wa Sheria.

Muda wa dhamana

30.-(1) Dhamana ya kuzingatia masharti ya mazingira iliyowekwa itakuwa halali mpaka itakaporudishwa au kutaifishwa.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo (1), dhamana iliyowekwa, haitarudishwa au kutaifishwa hadi Baraza litakapojiridhisha kwamba mwekezaji amezingatia mpango wa ufungaji wa mradi.

Kutunza

31. Baraza au mwekezaji atatunza kumbukumbu za

kumbukumbu

taarifa zinazohusu mradi ili kurahisisha utekelezaji wa masharti ya Kanuni hizi.

Msamaha

32. Masharti ya Kanuni hizi hayatahusisha miradi ya kutoa huduma inayotekelezwa na Serikali.

Makosa na adhabu

33. Mwekezaji ambaye anakiuka sharti lolote la Kanuni hizi, ambalo adhabu mahususi haijatolewa, anatenda kosa na akitiwa hatia, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi bilioni moja au kutumikia kifungo kwa muda usiopungua miezi mitatu na usiozidi miaka saba au vyote.

Rufaa

34.-(1) Mtu ambaye hajaridhishwa na uamuzi uliotolewa chini ya Kanuni hizi, anaweza kukata rufaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria.

(2) Endapo rufaa chini ya kanuni ndogo ya (1) inaenda kwa Waziri, Rufaa hiyo itawasilishwa ndani ya siku thelathini kuanzia siku ya kutolewa uamuzi unaokatiwa rufaa na itakuwa kwa njia ya barua itakayoambatishwa na nakala ya uamuzi na nyaraka nyingine ambayo Waziri anaweza kuhitaji.

(3) Waziri atatakiwa kutoa uamuzi wake ndani ya siku kumi na nne kuanzia siku ya kupokelewa kwa rufaa.

(4) Waziri atatakiwa kumjulisha mleta rufaa uamuzi wake na sababu za uamuzi huo ndani ya siku saba kuanzia siku aliyotoa uamuzi.

Mamlaka ya kutoa miongozo na maelekezo ya kisera

35. Waziri, baada ya kushauriana na wizara husika za kisekta, anaweza kutoa miongozo au maelekezo ya kisera ili kuwezesha utekelezaji bora wa Kanuni hizi.

Dhamana inayosimamiwa na sheria za kisekta

36.-(1) Sheria zozote za wizara za kisekta au taasisi zinazosimamia uwekaji wa dhamana yoyote inayohusiana na mazingira zitatakiwa kuzingatia masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), sekta au taasisi yoyote iliyopokea dhamana kwa ajili ya ufungaji salama,

uboreshaji wa eneo la mradi na urejeshaji wa mifumo ikolojia itapaswa kumtaarifu Waziri kuhusu aina, kiasi na usimamizi wa dhamana au sehemu ya dhamana hiyo iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mazingira.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

(*Limetengenezwa chini ya kanuni za 2, 8(1), 14(6), 22(3), 24,27 na 29)*

ORODHA YA MIRADI INAYOHITAJI UWEKAJI WA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA

| Na. | MRADI | SHUGHULI | MUDA WA KUWASILISHA MPANGO WA KINA WA KUFUNGA MRADI (baada ya kuanza kwa mradi) | KUHUISHA MPANGO WA KUFUNGA MRADI | KIPINDI CHA UFUATILIAJI BAADA YA KUFUNGA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KILIMO | (a) Kilimo cha uwekezaji mkubwa (zaidi ya Hekta 100) | miaka 5 | miaka 5 | mwaka 1-3 |
| | | (b) Umwagiliaji katika maeneo makubwa ya Hekta zaidi au sawa na 500; | miaka 4 | miaka 5 | mwaka 1-5 |
| | | (c) Kilimo cha uwekezaji wa mazao ya aina moja (chakula na biashara) zaidi ya au sawa na hekta 100; | miaka 3 | miaka 5 | Miaka 3 -10 |
| | | (d) Kilimo cha maua zaidi au sawa na hekta 5; na | miaka 2 | miaka 5 | miak5 - 10 |
| | | | | | |
| | | (e) Viwanda vya Sukari | miaka 2 | miaka 5 | mwaka 1-3 |
| 2. | MISITU | (a) Uvunaji wa miti zaidi au sawa na hekta 5; | mwaka 1 | miaka 3 | mwaka 1- 5 |

*Tangazo La Serikali Na. 388 (Linaendelea)*

| Na. | MRADI | SHUGHULI | MUDA WA KUWASILISHA MPANGO WA KINA WA KUFUNGA MRADI (baada ya kuanza kwa mradi) | KUHUISHA MPANGO WA KUFUNGA MRADI | KIPINDI CHA UFUATILIAJI BAADA YA KUFUNGA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) kutibu mbao kwa kutumia kemikali: | mwaka 1 | miaka 5 | miaka 5 - 10 |
| | | | | | |
| 3. | UVUVI | (a) Uvuvi mkubwa wa Samaki unaojumuisha uvunaji wa samaki kamba zaidi au sawa na tani 50 kwa siku; | Miaka 2 | miaka 5 | miaka 3 - 5 |
| | | (b) Ufugaji mkubwa wa samaki | miaka 2 | miaka 5 | miaka 2- 3 |
| | | (c) Uchenjuaji na uhifadhi mkubwa wa Samaki unazidi tani 50 kwa siku. | miaka 3 | miaka 5 | miaka 2 |
| | | (d) Samaki watokanao na vinasaba vilivyoboreshwa na viumbe wengine wa majini. | miaka 3 | miaka 5 | miaka 3- 5 |
| | | | | | |
| 4. | NISHATI | (a) Uwekezaji wa Umeme unaotokana na nguvu ya Joto unaozidi au sawa na 50 Megawati; | mwaka 1 | miaka 5 | miaka 1- 3 |
| | | (b) Kinu cha kuzalisha umeme wa nuklia | mwaka 1 | miaka 3 | miaka 5-15 |
| | | (c) Mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe | mwaka 1 | miaka 3 | miaka 5-10 |
| | | | | | |
| 5. | VIWANDA VYA UCHENJUAJI (Nguo, Ngozi, Mbao, Karatasi etc) | (a) Uzalishaji wa nyuzi-viwandani | mwaka 1 | miaka 3 | mwaka 1 –3 |
| | | (b) Usindikaji wa ngozi; mitambo jumuishi | mwaka 1 | miaka 3 | mwaka 1-3 |
| | | (c) Usindikaji wa | mwaka 1 | miaka 3 | mwaka 1-3 |

*Tangazo La Serikali Na. 388 (Linaendelea)*

| Na. | MRADI | SHUGHULI | MUDA WA KUWASILISHA MPANGO WA KINA WA KUFUNGA MRADI (baada ya kuanza kwa mradi) | KUHUISHA MPANGO WA KUFUNGA MRADI | KIPINDI CHA UFUATILIAJI BAADA YA KUFUNGA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | tumbaku; | | | |
| | | (d) Viwanda vya uzalishaji wa karatasi | mwaka 1 | miaka 3 | mwaka 1-3 |
| | | | | | |
| 6. | VIWANDA VYA KEMIKALI | (a) Uzalishaji wa viuatilifu kemikali nyingine hatarishi. | mwaka 1 | miaka 2 | mwaka 1– 5 |
| | | (b) Maghala makubwa ya kuhifadhi viuatilifu | mwaka 1 | miaka 2 | Mwaka 1–5 |
| | | (c) maghala makubwa ya kuhifadhi mafuta na kemikali zitokanazo na uchakataji wa petroli | mwaka 1 | miaka 2 | Mwaka 1–5 |
| | | (d) uzalishaji wa madawa ya binadamu | miaka 2 | miaka 5 | Mwaka 1-3 |
| | | (e) Uzalishaji wa rangi na ving'arishi; | mwaka 1 | miaka 2 | Mwaka 1 –5 |
| | | (f) Mitambo mikubwa ya kungeneza sabuni na; | miaka 3 | miaka 6 | Mwaka 1-3 |
| | | (g) Uzalishaji wa mbolea za viwandani. | miaka 3 | miaka 6 | Mwaka 1-3 |
| | | | | | |
| 7. | VIWANDA VYA UZIDUZI (UCHIMBAJI) | (a) Kuchimba na kuchejua Madini (Migodi Mikubwa na Migodi ya Kati). | mwaka 1 | miaka 3 | Miaka 5 – 30 |
| | | (b) Madini ujenzi (Mawe, Mchanga, Kifusi) | mwaka 1 | miaka 2 | Mwaka 1 –5 |
| | | (c) Mitambo ya uchenjuaji vitu visivyo vya hidrokaboni na isiyo-haidrokaboni (Oksijeni, Heliam, na Kabonidaioksaidi) | mwaka 1 | miaka 2 | Mwaka 1 –5 |

*Tangazo La Serikali Na. 388 (Linaendelea)*

| Na. | MRADI | SHUGHULI | MUDA WA KUWASILISHA MPANGO WA KINA WA KUFUNGA MRADI (baada ya kuanza kwa mradi) | KUHUISHA MPANGO WA KUFUNGA MRADI | KIPINDI CHA UFUATILIAJI BAADA YA KUFUNGA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Mitambo ya uzalishaji wa diezeli asilia | mwaka 1 | miaka 2 | Mwaka 1 –5 |
| | | (e) Haidrokaboni (Uzalishaji, usafirishaji, mabomba, utunzaji na uhifadhi wake). | mwaka 1 | miaka 3 | Miaka 5-30 |
| | | | | | |
| 8. | VIWANDA VINAVYOZALISHA BIDHAA ZISIZO ZA METALI | Uzalishaji wa Saruji | miaka 2 | miaka 5 | mwaka 1-5 |
| | | | | | |
| 9. | UMEME NA VIFAA VYA KIELEKRTONIKI | Uzalishaji wa betri na Urejelezaji wa betri chakavu | mwaka 1 | miaka 3 | mwaka 1-5 |

JEDWALI LA PILI

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8 (2)*)

MPANGILIO WA MPANGO WA KINA WA UFUNGAJI WA MRADI

| SURA | MAUDHUI |
|---|---|
| Ukurasa wa juu | utajumuisha jina la mradi, jina na anwani ya mwekezaji/mtaalamu wa mazingira aliyesajiliwa na tarehe ya kuwasilisha |
| yaliyomo | itaJumuisha orodha ya michoro |
| Utangulizi | Utajumuisha taarifa za usuli, Mawanda na madhumuni ya Mpango wa ufungaji wa mradi. |
| Maelezo ya mradi | yatajumuisha miongoni mwa mengine, eneo la mradi, sifa za eneo la mradi, aina ya shughuli au michakato, taarifa na data za msingi, uchambuzi wa mifumo ya usimamizi wa mazingira; |
| Tathmini ya hatari na Mpango wa Usimamizi | itajumuisha utambuzi wa hatari, tathmini na usimamizi, |
| Ushirikiano wa wadau | Ufungaji wa mradi unapaswa kuwa mchakato wa mashauriano, wadau muhimu watambuliwe na kushirikishwa |
| Mbinu na njia za ufungaji wa mradi | Uchambuzi wa njia mbalimbali za kufunga mradi, kuweka wa vigezo vya kukamilisha ufungaji wa mradi, ukusanyaji na uchambuzi wa data za ufungaji miradi inayoungwa mkono na tafiti maalumu, inapobidi; |
| Mpango wa utekerezaji na ufuatiliaji wa ufungaji wa mradi | Itajumuisha hata zilizopo wakat wa kufunga mradi kwa dharula, mpango wa dharura wakati wa kipindi cha kufunga mradi. |
| Masharti ya fedha | Ikijumuisha uchanganuzi wa gharama ya Dhamana ya Uzingatiaji wa Masharti ya Mazingira. |
| Marejeleo na viambatisho | |

*Tangazo La Serikali Na. 388 (Linaendelea)*

___________

JEDWALI LA TATU

___________

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 11(2)*)

CHETI CHA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA

*Uthibitisho wa Dhamana iliyopokelewa*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KANUNI ZA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA ZA MWAKA 2024**

__________

**CHETI CHA DHAMANA YA KUZINGATIA MASHARTI YA MAZINGIRA**

_________

(*Kimetolewa chini ya kanuni ya 12 (2)*)

_________

Cheti Na...................……

Hii ni kuthibitisha kwamba

………………..................................……wa S. L. P ……….....……………… ameweka Dhamana Kuzingatia Masharti ya Mazingira kwa njia ya ......................................................................…… *(aina ya Dhamana iliyowekwa*) kwa ................................................ (*Jina la Mtoa Dhamana*) ....................................................................................................

Cheti hiki kinathibitisha kwamba Mwekezaji tajwa, ameweka Dhamaba ya Uzingatiaji wa Masharti ya Mazingira ili kudhamini mradi ulioidhinishwa…………………………………………………………………………………
*(Jinala mradi na mahali unapotekelezwa)*

Cheti hiki ni kuthibitisha kwamab, kampuni haitafuta dhamana iliyowekwa mpaka Mhifadhi wa Dhamana atakapojiridhisha na hali ya mazingira katika eneo la mradi

Cheti hiki hakitakuwa halali kwa mradi wowote unaofuata.

*Masharti na vigezo vya Cheti hiki yameainishwa nyuma ya Cheti hiki.*

Jina………………………….………………………..….

Saini …………………..…………………………......

Tarehe…………………….…………………………..

*Waziri mwenye dhamana ya mazingira*

Dodoma,
……..……..., 2024

SELEMANI SAIDI JAFO
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira*